



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA



OFISI YA:-

MKUU WA POLISI
WILAYA KARIAKOO,
P.O. BOX 9140,
DAR ES SALAAM.

Kumb Na.CGB.795/895/01/27

22/04/2025

KATIBU CHADEMA
JIMBO LA ILALA
DAR ES SALAAM

YAH: KUTOA TAARIFA YA MKUTANO WA HADHARA

Tafadhalii husika na somo tajwa hapo juu .

2. Nimepokea barua yako yenyeku kumb CPM/111/2025/ MKT/01 ya tarehe 16/04/2025
yahusika.

3. Kwa mujibu wa sheria mikutano ya kisiasa imeruhusiwa kufanyika maeneo
mbalimbali.

4. Hivyo eneo mlilo litaja la kufanya mikutano huo la Mtaa wa Nyamwezi na Mkunguni
Kariakoo ni eneo lenye watu wengi wanaondelea na shughuli za kibiashara, ili kulinda
haki za watu wenye shughuli zingine tunashauri mikutano wenu huo wa hadhara
ukafanyike kwenye viwanja vya wazi ambavyo haviwezi kuleta hatari za uvunjifu wa
amani.

5. Nawasilisha tafadhalii.

**J. E. JOSEPH-SSP
MKUU WA POLISI (W) KARIAKOO
DAR ES SALAAM.**

Nakala:
RPC (M) ILALA- Kwa taarifa.
MKUU WA (W) ILALA –Kwa taarifa
DSO ILALA- Kwa taarifa

**MKUU WA POLISI
WILAYA YA KARIAKOO**



KATIBU CHADEMA

JIMBO LA ILALA,

P. O. Box 31191

DAR ES SALAAM

April 22, 2025

Kumb: CDM/ILL/2025/MKT/02

MKUU WA POLISI

WILAYA YA KARIAKOO

S.L.P 9140

DAR ES SALAAM

YAH: MAJIBU KUHUSU BARUA YA KUHAMISHA ENEO LA MKUTANO WA

HADHARA JIMBO LA ILALA.

Tafadhalii husika na mada tajwa hapo juu.

CHADEMA Jimbo la Ilala tumeona barua yako yenyen kumb CGB.795/895/01/27

ikieleza kuhamisha mkutano wa hadhara utakaohutubiwa na Makamu
Mwenyekiti Taifa Mh.JOHN HECHE leo April 22, 2025 katika eneo la mtaa wa
Nyamwezi na Mkunguni.

Kwanza napenda kuweka wazi kuwa hatukubaliani na uamuzi wa kuhamisha
mkutano huu kwa sababu zifuatazo,

1. Taarifa ya mkutano huu tumetoa polisi tarehe 16.04.2025 siku sita
zilizopita na kipindi chote jeshi la Polisi mlikaa kimya.

2. Taarifa ya Kuhamisha mkutano huu imekuja masaa machache kabla ya
kuanza mkutano na hakukua na udharura huo.Maandalizi yamefanyika
kwa asilimia mia moja ikiwa ni pamoja na Matangazo, Jukwaa na
Mapambo

3. Eneo hilo limekua likifanyiwa mikutano na vyama vyote ikiwemo CCM na
hatukuwahi kuona zuio au hamisho la aina yotote

4. Eneo hilo pamoja na mikutano kufanyika,hakuna shughuli zozote
zimewahi kusimama na halijawahi kupungua watu

5. Ni wajibu wa Jeshi la polisi kuhakikisha usalama katika mkutano huu na
sio vinginevyo.

Kwa sababu hiyo,tunasisitiza kuwa mkutano huu utaendelea kama kufanyika
kama ulivyopangwa awali.Tunasihi Jeshi la polisi kushirikiana nasi kwa lengo la
kuhakikisha mkutano unafanyika kwa amani na utulivu katika eneop
tulilopanga.

Wako katika ujenzi wa Demokrasia na Maendeleo

ELIZABETH MAMBOSH

KATIBU WA JIMBO LA ILALA